

Pambazuko

Toleo Namba 33

Jumatatu Aprili 3-9, 2023

**Uk.
10-11**



- *Tanzania bado shamba kubwa la bibi*
- *Wananchi wasema 'stupid' haitoshi*

**Walionyofoa
kizazi cha
mtoto
kunyongwa**

Uk. 5

**Uk.
19**

**Katoliki
wakana
kueneza dini
kimabavu**

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Rais Samia achukue hatua kali

WIKI iliyoupita - Jumatano, Machi 29, Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alionyesha hasira zake kwa umma kwa maneno makali.

Akipokea ripoti ya Mkguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali (CAG), jijini Dar es Salaam, Rais Samia alikerwa mno na kuwepo kwa kila dalili za rushwa, wizi na ubadhirifu ambazo zimesheheni ndani ya taarifa hiyo aliyokabidhiwa.

Katika uongozi wake wa miaka mwili, kwa mara ya kwanza, Watanzania na dunia walishuhudia namna ambavyo Rais Samia hapendi rushwa, wizi na ubadhirifu. Alifoka huku sura yake ikionekana "kuvaa" hasira.

Rais Samia alifika wakati akatumia maneno makali ya Kiingereza; "stupid" - akimaanisha upumbavu mkubwa kwa baadhi ya watendaji wa serikali ambao wamekuwa wakishindwa kutumia uzalendo katika kuwajibika, badala yake wamekuwa wakiamini dhamana zao ni chumo lao kwa manufaa binafsi.

Pamoja na Pambazuko kupongeza hasira hizo za Rais Samia, bado tunaamini kwamba hasira pekee hazitoshi kuwakemea Watanzania wengi kuacha rushwa, kujihusisha na ubadhirifu na hata matumizi mabaya ya dhamana walizokabidhiwa kwa niaba ya wananchi.

Rais Samia amekuwa sehemu ya utendaji wa serikali kwa muda mrefu, hivyo tunaamini anatambua wapi kuna mianya mingi ya rushwa ubadhirifu na uchafu mwingine ambao unachafua taswira ya serikali yake kwa umma wa Waanzania

na dunia.

Kimsingi, wanaotenda maovu hayo, wanamchongea Rais Samia kwa wananchi, na kumuonyesha kwamba ni kiongozi asiyechukua hatua kunapotokea uchafu katika utendaji wa serikali.

Kama ambavyo wananchi wengi wanapendekeza Rais Samia kuchukua hatua kali; ikiwamo kuwatimua kazini na kuwafungulia mashtaka wote wanaiba mali za wananchi, nasi katika Pambazuko tunasisitiza kiongozi huyo wa nchi yetu kuchukua hatua kwa wote wanaomhujumu.

Kuiba mali ya umma ni dhambi kubwa mno, kwani inahusisha kudhulumu haki za idadi kubwa ya wananchi. Kuiba fedha za maendeleo maana yake ni kwamba mwizi huyo anakwamisha ujenzi wa barabara, anachelewesha kama siyo kuzuia kabisa ununuzi wa dawa katika hospitali na anakwamisha kuimarika kwa elimu ya watoto wetu.

Mwizi wa mali ya umma ni mbaya mno. Ni sawa kabisa na kua watu kwa manufaa ya mtu binafsi na gharama za wengi.

Ndiyoo maana katika nchi zingine, mwizi wa mali ya umma hupigwa risasi hadharani ili kuwa fundisho kwa watendaji wengine wenye tamaa ya kupata utajiri wa harakaharaka kwa mgongo wa fedha za maendeleo ya umma.

Pambazuko linamuomba Rais Samia sasa kuwa mkali zaidi kwa wezi wote wa mali ya umma na wale wanaotumia vibaya dhamana zao.

Sisi Pambazuko tuko tayari kumsaidia kwa njia tunazoweza ili kuifanya Tanzania ikome kuonekana kuwa shamba la bibi, ambamo kila anayepita jirani, anakula mazao bila kukemewa.

TANZANIA TUITAKAYO...



Makamu wa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana (kushoto) akiwa na Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Rais (mstaafu), Jakaya Kikwete wiki iliyopita wakati wa hafla ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyomwandalia Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris jijini Dar es Salaam. Kamala alikuwa na siera ya siku tatu nchini Tanzania. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



“Serikali inafanya kila linalowezekana kuwapa elimu, lakini uamuzi wa kuitumia elimu hiyo ni wenu, tambueni kuwa upo mzigo mkubwa sana wa kuongoza hii nchi unawasubiri, someni kwa bidii sana, mpate maarifa na ufahamu mkubwa. Msituangushe” - Benjamin William Mkapa, Rais wa Tanzania (1995 – 2005). Mkapa sasa ni marehemu.

Tafakuri

Dhambi kubwa ni kuogopa kutetea haki

Na Plato Hekimachius

KUNA mambo yanatokea mara kwa mara na kujijengea kanuni kuwa ni ya kawaida na yataendelea kutokea. Yamekuwapo katika harakati za kupigania uhuru, yakaendelea baada ya uhuru na yanaendelea hata sasa, zaidi ya nusu karne tangu Tanzania ipate uhuru. Haya mambo yanahitaji kujengewa mnara wa kumbukumbu na yakubaliwe kuwa ni sehemu muhimu ya historia ya ukombozi. Nitajadili matatu kwa ufupi.

Kwanza, ukipenda madaraka, usiogope kifungo.

Ukiwa nje ya mfumo na unapigania ili uingie madarakani, ni bora kujiandaa kisaikolojia kuwa kifungoni. Aidha, ukiwa madarakani na unapenda hayo madaraka, ujiandae kisaikolojia kuwa ipo siku utajikuta kifungoni ukiwa madarakani au hata baada ya kutoka madarakani.

Uwepo wa kinga za kisheria ndani ya katiba za nchi, hauzuii mtu kuwekwa kifungoni. Hii ni kwa sababu hata wale wasiokuwa madarakani, wana kinga isiyoundikwa kwenye katiba, lakini walio madarakani huzipuua na kuwaweka kifungoni. Mnyumbuliko huu ndio hujenga mazoea ya unasaba kati ya kifungo na madaraka. Viongozi wa kisiasa waliofanikiwa katika maisha ya kisiasa ni wale waliokubali kuwa kifungo na madaraka ni ndugu wa damu.

Pili, ukipenda kutetea haki, kubali kudhalilishwa.

Haki ni kinyume cha dhuluma. Kwa hiyo ukitetea haki unaingia katika vita na dhuluma. Mfumo wa dhuluma una watetezi wake pia na wako katika tasnia zote. Kwa hiyo ukigusa dhuluma, watetezi wake huinuka na kupambana na watetezi wa haki. Njia maarufu ya kukabiliana na watetezi wa haki ni kuwadhalilisha kwa uwongo, kuwaita majina mabaya, na hata kuwatishia kifo.

Hali hii huwaweka watetezi wa haki wote kuwa tayari kutukanwa na kudhalilishwa wakati wowote. Udhaliishaji wa watetezi unahitaji kujengewa mnara wa kumbukumbu kwa



Rais Samia Suluhu Hassan

sababu ni sehemu muhimu isiyobadilika. Watetezi wa haki duniani kote yawapasa kujiandaa kisaikolojia kukabiliana na kuizoea hali hii.

Tatu, ukipenda Habari za uchunguzi, uwe tayari kufunguwa.

Habari za uchunguzi katika tasnia ya habari ni kiungo muhimu kinachoozgeza heshima ya tasnia hiyo. Lakini, heshima hiyo ina gharama kubwa kwa waandishi. Serikali nyingi pamoja na kujinadi kuwa za kidemokrasia, lakini linapofika suala la habari za uchunguzi, serikali hizo hutumia sheria kadamizi kuzuia habari hizo.

Mbinu zinazotumiwa na serikali hizo ni pamoja na utaratibu wa 'kulesenisha' habari, kufanya usanii wa kukiri uwepo wa sheria kandamizi, lakini bila kuchukua hatua ya kuzifuta, na kutumia wana habari wenyewe kuwa wasimamizi wa mifumo kandamizi ya habari za uchunguzi. Kilele cha dhuluma dhidi ya habari za uchunguzi ni uwepo wa kisingizio cha uchochezi na kuhatarisha usalama wa nchi.

Kwa hiyo, ukiwa mwandishi wa habari za uchunguzi ni vyema kuwa tayari kufunguwa, kufunguwa, kufilisiwa na kuvurugwa kimapato.

Mnara huu unahitajika kujengwa ili kuthibitisha uwepo wa uhasama wa kudumu katika habari za uchunguzi na serikali zisizopenda uwazi na utawala wa sheria.

Walionyofoa kizazi cha mtoto kunyongwa

Na Mwandishi WETU

MBIO na kukuru-kakara za kusaka utajiri wa haraka, hatimaye sasa zinawaweka watu wawili kwenye orodha ya watu wanaosubiri kunyongwa hadi kufa.

Watu hao, kwa kufanya ushirika wa kishetani, walimuua binti wa miaka minne (4), Samira Said, baada ya mmoja wao kumteka, na kumpeleka kwa mwenzake ambaye alifanya unyama kwa kuingiza mkono wake kwenye sehemu zake za siri za mtoto na kunyofoa via vyote vya uzazi na baadaye kuutupa mwili wake.

Kutokana na kuthibitika pasipo shaka, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Joachim Tinganga, Ijumaa iliyopita, Machi 31, 2023, aliwahukumu Richard Kimweri (43) na Mbwana Makamba (47) kunyongwa hadi kufa.

Wawili hao; Kimweri na Makamba imethibitishwa na mahakama kwamba walifanya unyama huo kwa kushirikiana, ili kufanikisha lengo lao kubwa la kupata utajiri.

Mahakama ilielezwa kwamba wawili hao walifanya kitendo hicho cha kuteka, kutesa na hatimaye kuuwa Juni 20, 2016 katika eneo la Makaburi ya Banani, Unga Limited, nje kidogo ya Jiji la Arusha.

Ilielezwa kuwa Kimweri ambaye alikuwa mlinzi wa makaburi hayo, alikwenda kwa mganga, ambaye ni Makamba na kumweleza nia yake ya kupata utajiri wa haraka kupitia njia za uchawi ambazo, inaelezwa kuwa Makamba, kwa kuwa mganga wa kienyeji, alikuwa na "utaalamu" nazo.

Mahakama ikaelezwa kwamba Makamba alimtaka Kimweri kuleta mtoto mdogo wa kike ambaye hajavunja ungo, ili iwe njia ya kufikiwa kwa matamano yake ya kuwa tajiri kwa haraka na bila "kutoa jasho jingi."

Ikaelezwa kwamba Kimweri baada ya kutakiwa kuleta mtoto, alienda nje ya eneo lake la kazi, Makaburi ya Baniani,



Mkuu wa Jeshi la Polisi, Camillus Wambura

na kumrubuni Samira, ambaye alikuwa miongoni mwa watoto waliokuwepo wakicheza.

Kwamba Kimweri alimrubuni Samira kwamba amfuate ili akampatie pipi na atamrudisha hapo kwa wenzake, lakini tangu siku hiyo, binti huyo hakuonekana tena.

Maelezo ya mashahadi 12 wa upande Jamburi walieleza kwamba baada ya Kimweri kuondoka naye na kutokomea eneo la Daraja II, alimfikisha kwa mganga – Makamba ambaye alimpakata na kumvua nguo zake na kuingiza vidole vyake sehemu za siri za Samira na kumyofoa via vya uzazi.

Nje ya mahakama, Pambazuko lilielezwa kwamba Samira, alizibwa mdomo na kipande cha kanga, ambapo Kimweri alifanya kazi hiyo, huku Makamba akinyofoa viungo hivyo vya Samira. Haikufahamika mara moja kipande hicho cha kanga kilikuwa cha nani, ingawa mazingira yanaonekana kilitolewa ndani ya chumba cha "uchawi" cha Makamba.

Ripoti ya uchunguza wa vinasaba (DNA) ilionyesha kwamba sampuli zilizochukuliwa eneo jirani na sehemu za siri za Samira zilioana na mabaki ya damu yaliyopatikana kwenye kucha za Makamba na Kimweri.

Habari

RC wakana kueneza dini kimabavu

Na Amani JUMA

MIAKA 500 baada ya makuwadi wa ukoloni na utumwa kutumia “Matamko ya Kipapa” kama leseni ya kuhalalisha sera zao, sasa Kanisa Katoliki limekana kuhusika na sera hizo.

Alhamisi iliyopita, Machi 30, 2023, Vatican ilitoa tamko linaloeleza kwamba, “sera hizo siyo sehemu ya mafundisho ya Kanisa Katoliki.”

Tamko hilo, lenye kurasa mbili na maneno 817, linasisitiza kwamba, “siku zote Kanisa Katoliki limetumia misamati iliyonyooka kutetea heshima ya kila binadamu.”

Tamko linafafanua kuwa, “Matamko ya Kipapa” yaliyotumiwa na wale walioitwa na kanisa hilo kuwa ni makuwadi wa ukoloni na utumwa yalikuwa ni “maandiko ya dharula ya Kipapa yanayokihusu kipindi maalum cha kihistoria yakijadilia masuala ya kisiasa ya wakati huo, na ambayo hayajawahi kuwa sehemu ya msimamo rasmi wa imani Katoliki.”

Lakini pia, tamko hilo linakiri kwamba, katika kipindi hicho kuna “Matamko ya Kipapa” ambayo hayakuzingatia kwa ukamilifu “heshima ya ubindamu na haki za watu asilia” katika Afrika, Amerika na Asia.

Tamko linaongeza kwamba, kwa sababu hiyo, kuna “Matamko ya Kipapa yaliyonyumbulishwa na wakoloni ili kukidhi matakwa yao ya kisiasa yaliyokiuka haki za watu asilia katika duni mpya, tena pasipo upinzani kutoka kwa uongozi wa Kanisa Katoliki.”

Hivyo, “ni haki kutambua makosa haya, kukiri maumivu na madhara makubwa yaliyotokana na sera za kuwatakatifuza kibabe wakazi asilia, na kuomba msamaha,” linahitimisha tamko la Vatican.

Kuanzia karne ya 15, Ureno, mataifa ya Ulaya yalifadhili safari za upelezi wa fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii katika “dunia mpya,” ambayo yalitawaliwa na kusambaa kwa dini maeneo mbalimbali ya dunia.



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Jude Ruwaichi

Zama hizo ziliitwa kipindi cha upelelezi, kipindi cha ugunduzi au kipindi cha makabiliano kati ya wakazi asilia katika dunia mpya na wapelelezi wa kutoka Ulaya na Amerika wakiwamo Bartolomeu Dias, Vasco da Gama, na Christopher Columbus.

Ziara za wapelelezi hao ziliwafungulia milango wazungu waliokuja kufanya utekaji wa ardhii, ukoloni na biashara ya utumwa katika Afrika na Asia.

Aidha, ziara za wagunduzi hawa ziliuchochea uongozi wa Kanisa Katoliki wa wakati huo kuandaa “Matamko ya Kipapa” yaliyohimiza na kuhalalisha kutekwa kwa wenyeji waliogunduliwa na wapelelezi, kunyakuliwa kwa ardhii yao, na hatimaye mateka na mali zao kugeuzwa mali ya serikali za Ulaya zilizowatuma wapelekezi hao.

Kwa mfano, “Tamko la Kipapa” liitwalo “Dum Diversas,” lililoandikwa na Papa Nicholas V mwaka 1452, lilitoa baraka kwa Serikali ya Ureno kuhakikisha kwamba, watu waliogunduliwa katika “dunia mpya” na kuukataa Ukristo, kubaki kuwa “watumwa wa milele.”

Matamko ya Kipapa mengine yanayolalamikiwa na wanazuoni ni tamko la Papa Nicholas V, liitwalo “Romanus Pontifex (1455)” na tamko la Papa Alexander VI liitwalo “Inter Caetera (1493).”

Ruto, Raila kumaliza tofauti zao

**Na Mwandishi WETU,
Kenya**

HABARI zilizotufikia jana usiku wakati tunakwenda mitamboni, zinaeleza kwamba maandamano ya kila Jumatatu yaliyokuwa yaendeleo leo, yamesitishwa.

Hii inatokana na kauli aliyotoa Rais William Ruto kwa kiongozi wa upinzani, Raila Odinga, ambaye amekubali kusitisha maandamano hayo.

Sasa viongozi hao wamepanga kukutana na kujadiliana namna nzuri ya kukoa Kenya na machafuko yanayoweza kujitokeza.

Awali, mnyukano wa kuonyeshana nguvu za kisiasa kati ya Rais William Ruto na mpinzani wake, Raila Odinga, unaonekana kuendelea kukua baada ya kila mmoja kueleza “kutotishwa” na mwingine.

Tayari Raila amesema kamwe hatazuiwa na yeyote kuandamana na kuwapigania Wakenya ili wawe na maisha bora, huku Rais Ruto akiapa kumdhhibi mpinzani wake ili “asimwaribie nchi.”



Raila Odinga

“Mimi nimekuwa na maisha ya muda mrefu kuwapigania Wakenya na siwezi kuchoka hadi hapo wananchi wetu watakapokuwa na maisha yenye unafuu. Hakuna wa kunikataza kuandamana kwa kuwa ni haki ya kikatiba kwa kila Mkenya,” anasema Raila.

Rais Ruto amedai kuwa Raila ni “baba wa maandamano” na kwamba safari hii hataruhusiwa kufanya kile anachokieleza



Rais Ruto

kuwa ni “kuharibu Kenya na watu wake.”

Leo idadi kubwa ya wananchi wanatarajiwa kujitokeza kwa wingi kuendelea na maandamano yaliyoitishwa kila Jumatatu na Raila ili kuishinikiza serikali kuweka bei za ukomo kwa vyakula na hasa unga.

Katika hatua nyingine, Rais wa Chama cha Wahariri Kenya, Churchill Otieno amesema kuwa zipo taarifa kwamba serikali imepanga kuzima intaneti na vituo vyote vya utangazaji leo ikiwa ni njia ya kuzuia kusambaa kwa maandamano hayo.

Otieno jana alisema taarifa hizo zinaweza kuwa na ukweli kwani zinapatikana kutoka maeneo yenye uhakika kwa kiasi kikubwa.

“Endapo tetesi hizi zitakuwa na ukweli, hili litakuwa tukio baya zaidi kuwahi kutokea nchini kwa sababu linanyima haki ya kupata taarifa kwa wananchi,” amesema Otieno.

Kenya ambayo inaongozwa na Rais Ruto wa umoja wa Kenya Kwanza imekuwa katika msuguanu wa kisiasa na upande wa upinzani unaoongoza na Raila ambaye pia ni waziri mkuu (mstaafu).

Raila tangu kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa rais wa nchi hiyo uliofanyika mwaka jana, na baadaye kuyapinga mahakamani – ambako alibwagwa, bado anaendelea kuwa na msimamo kwamba Ruto hakushinda nafasi hiyo ya juu ya uongozi.

Marekani

Trump kizimbaki kwa uhalifu

Marekani

RAIS wa zamani wa Marekani ambaye ame kuwa akiandamwa na taarifa za kufanya vituko vingi hata kabla ya kuwa kiongozi wa taifa hilo tajiri zaidi kiuchumi na kivita duniani, Donald Trump, sasa anaongeza historia nyingine; anashitakiwa mahakamani.

Trump anakuwa rais wa kwanza kwenye historia ya Marekani kuwa kiongozi wa juu (akiwa madarakani ama amestaafu), baada ya kushtakiwa kwa tuhuma za kumhonga mwanamke mjia ili kuficha “dhambi zake.”

Rais huyo mwenye miaka 76 sasa, wiki ijayo huenda akapanda kizimbani kujibu mashtaka ya “kumfunga mdomo” muigizaji mmoja wa filamu za watu wazima, Stormy Daniels (44).

Inadaiwa Trump aliamua kupa fedha nyingi mwanamama huyo ili kumnyamazisha asitoe uhalifu wa kingono ambao alimfanyia miaka kadhaa iliyopita.

Inadaiwa kwamba Trump alifanya hivyo ili kumzuia mwanamama huyo kutoa siri ya kufanyiwa uhalifu wa kingono, muda mfupi kabla ya kiongozi huyo kutangaza nia yake ya kuwania uongozi wa juu wa taifa hilo.

Jopo la majaji katika Jiji la New York, wiki iliyopita walipiga kura ya kumshtaki Trump kwa makosa ya kumlipa muigizaji huyo kiasi cha dola za Marekani 130,000 (zaidi ya Shilingi milioni 300) ili “asitoboe siri.”

Inaeleza kwamba Trump wakati wa kampeni zake za kuwania urais za mwaka 2016, alimuita mwanamama huyo na kumpa kiasi hicho cha fedha ili “amlinde.”

Inasemekana kuwa mwanamama huyo alilipwa pesa hizo ili asiseme kama waliwahi kukutana kwao kimwili jambo ambalo mwanamama huyo anasema lilitokea miaka ya nyuma.

Akipanda kizimbani mwezi huu,



Donald Trump (Picha na CNN)

Trump atakuwa kiongozi wa juu kabisa wa Marekani katika historia ya nchi hiyo kushtakiwa mahakamani.

Mashtaka hayo ambayo yatatangazwa rasmi katika siku chache zijazo yamekuja wakati mwanasiasa huyo akiwania kugombea tena urais mwaka 2024.

Watu wa karibu na kiongozi huyo wanaeleza kwamba Trump anaonekana na “mfumo uliopo” ili kumzuia kuwania nafasi ya kuongoza tena katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwaka 2024.

Trump alishinda urais 2016 na kushindwa katika uchaguzi uliofuata wa mwaka 2020, baada ya kushindwa na rais wa sasa, Joe Biden.

Timu ya wanasheria wa Trump wanaeleza kwamba kesi hiyo ni ya kisiasa zaidi na kwamba wamejipanga kuhakikisha mwajiri wao “anaipangua.”

Mashirika ya habari ya kimataifa

Ng'wanamalundi na miujiza yenye maswali mengi - III

Na Ibengwe Shileki MAZEGE

WALIPOFIKA nyumbani, yule bibi akaamua kumwambia ukweli Igulu (Mwanamalundi) kuwa yule kifarua ni yeye mwenyewe. Aliamua kujibadili ili kuwapima uwezo wao wa kuvumilia magumu.

Kwa kuwa Igulu pekee ndio alioneshwa yuko imara, bibi yule alimtunuku dawa zitakazompa mvuto na nguvu katika ngoma zake. Wale vijana wawili walipitiliza hadi kwao bila kurudi tena kwa mganga.

Yule bibi mganga alimpa masharti kadhaa Igulu baada ya kumpa dawa. Bibi mganga alimzuia Igulu kumparaza mtu yeyote au kumnyooshea kidole. Iwapo atafanya hivyo, basi aliyeparazwa au kunyoosheba kidole atakufa hapohapo.

Igulu aliporudi kijijini kwake na kisha kucheza ngoma ya kwanza, baada tu ya kurudi kutoka kwa mganga, alishinda.

Kuna nyakati Igulu aliamua kucheza ngoma akiwa juu ya jiwe kubwa. Wakati akicheza ngoma hizo, kila anaponyanyua mguu wake, nyazo zake zilionekana kubaki juu ya mawe hayo.

Alama za nyayo za Igulu, zipo mpaka leo pale kijiji cha Nyandekwa, Wilaya ya Kahama, Shinyanga. Ni kama kilomita 10 tu kutoka makao makuu ya wilaya hiyo. Kuna nyakati Igulu alitengeza mashimo ya mchezo wa bao juu ya jiwe kwa kutumia kisigino chake. Ni alama ambazo pia bado zipo katika kijiji hicho chenye nayo zake.

Igulu aliposhinda mashindano ya ndani ya kijiji, akaamua kuomba kushindana na wapinzani wakubwa zaidi walioishi Kijiji cha Ng'wagala wilaya ya Maswa, Shinyanga. Hawa ni pamoja na



Ngwanamalundi

Samike, Ng'wanikinga, Ng'wanilog'ho na mwanamke mwenye nguvu za kiganga aitwae Gíndü Nkíma.

Hawa watu wanne walikuwa hawana mpinzani katika ngoma, lakini Igulu akajitosa kushindana nao, hatua ambayo iliwashangaza wengi hasa ikizingatiwa umri wake na zaidi uwezo wake uliotiliwa shaka.

Siku ya mashindano, Mwanamalundi alipofika kwenye uwanja wa mashindano, akafanya miujiza kwa kujirefusha kama ngongoti asiye na magongo yoyote yale na kisha akaanza kucheza huku akiwa ameficha uso wake kwa kitambaa cheusi kama kawaida yake.

Wakati anacheza ngoma akiwa ana urefu wa ngongoti, baadhi ya watu walijaribu kugusa na kuifunua miguu yake ili wajue kulikuwa kuna nini. Wote waliothubutu kuigusa walikufa baada ya muda mfupi. Katika ngoma hiyo, Gíndü Nkíma akatumia nguvu zake za kiganga kumrudisha Igulu (Mwanamalundi) kama alivyokuwa awali; yaani pasipo kurefuka kama ngongoti. Kwa kufanya hivyo, Mwanamalundi alipoteza pambano hilo.

Katika mashindano hayo, Mwanamalundi alishinda na kuwaduwaza washindani wake na hata watazamaji.

Habari**Wizi, wizi, wizi****Na Waandishi WETU**

TANZANIA itakoma lini kuwa shamba la bibi; kwamba kila anayepata nafasi ya uongozi anageuzi dhamana aliyopewa kuwa chumio la fedha kwa manufaa binafasi?

Hili ni swali ambalo idadi kubwa ya watu waliohojiwa na Pambazuko wameuliza walipohojiwa juu ya mtazamo wao kuhusu Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere – kwa mwaka 2021/22.

Ripoti hiyo iliyowasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan Jumatano iliyopita – Machi 29, 2023 jijini Dar es Salaam ilibainisha kuwepo kwa wizi na ubadhirifu kwa fedha za Tanzania ambazo zinapaswa kusaidia wananchi wote, lakini zinaishia kwa watu wachache, hasa watumishi wa serikali, halmashauri, mashirika na taasisi za serikali.

Tangu kuanza kusoma kwa muhtasari wa ripoti hiyo, kulionekana kuwepo kwa dalili za wizi mkubwa wa fedha zilizopangwa kuwa za maendeleo, lakini kuishia mifukoni mwa wasimamizi wa fedha hizo.

Maeneo yaliyoguswa na CAG Kichere ni mengi, lakini yaliyothibitika kutikisa ni kuwepo kwa uthibitisho na kuwepo kwa dalili za wizi karibu kila eneo alilogusa CAG.

Mbali na wananchi kukerwa na wizi na “michongo” mingine ya wizi, kwa mara ya kwanza, akiwa hadharani, Rais Samia alisikika na kuonekana dhahiri shahiri amekasirika na hata kutumia maneno yasiyozoeleka kutoka kinywani mwake.

Kuonyesha hasira zake, baada ya kukwera zaidi alitumia hadi neno la Kiingereza – stupid (likiwa na maana ya upumbavu) – kuonyesha hasira zake waziwazi.

RAIS Samia alikwera zaidi baada ya kubaini kuwepo kwa kile alichoeleza kuwa ni upumbavu wa baadhi ya watendaji wa serikali katika ununuzi wa



CAG Kichere CAG Kichere

ndege kubwa ya mizigo inayotarajiwa kuwasili hivi karibuni nchini baada ya matengenezo.

CAG alibainisha mazingira ambayo yanatia shaka kwa kuwepo ongezeko kubwa la fedha katika matengenezo ya ndege hiyo. Awali gharama zilizielezwa kuwa ni dola milioni 37, lakini hivi karibuni Ikulu ikapeleleka taarifa za kupanda kwa gharama hizo kufikia dola milioni 86. Ongezeko la dola milioni 49.

“Invoice (ankala ya kudai) imekuja tunatakiwa kulipa dola milioni 86; unauliza mkataba ulisemaje? Hii imetokea wapi? Ohoo vifaa vimepanda bei, vipi mkataba wetu ulisemaje?”

“Bado aliyepokea anakuletea serikali hii ilipwe ndio invoice tumepokea; stupid, ulipokea umechukua hatua gani, umeuliza? Umefanya nini ukilitazama kwa undani hili ongezeko limeanzia huku ndani kuna watu wameongea huko,” alifoka na kuongeza:

“Hatuwezi kwenda hivyo nadhani hawa wanaopokea hizo invoice wakazileta kwa raha zao kabisa serikalini... hawa

Wizi, wizi, wizi

Inatoka Uk. 10

watupishe, hawafai kuwa kwenye hizo nafasi kama wanafaa angepokea huko akahoji.

“Baada ya kuhoji akasema nilipokea hivi, nimeambiwa hivi, lakini bado nimeomba tufanye hivi huyu unamuelewa, lakini mtu anapokea kwa raha zake tu analeta serikalini kuna hiyo ‘invoice’ imekuja vifaa vimeongezeka baada ya Covid... pumbavu haiwezekani, mawaziri tusaidieni; ‘over invoicing’ (ankala za madai zinazowekwa bei kubwa zaidi ya uhalisia) zipo nyingi sana.”

Hata hivyo, wananchi wengi wanahimza kwamba “stupid” aliyoitoa Rais Samia haitoshi, lazima achukue hatua kali za kukoa fedha za wananchi na maendeleo yao.

Jumaa Ally, aliyejitambulisha kwa Pambazuko kuwa mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema kufoka kwa Rais Samia, hakutakuwa na maana ikiwa wahusika wa wizi na ubadhirifu anawafahamu.

“Wizi kutamka stupid, haitatosha na Watanzania wengi, hasa watumishi wa serikali na taasisi zake, wamezoea wizi na ubadhirifu wa kutisha, anatakiwa kuchukua hatu za kufukuza, kufungua kesi za uhujumu uchumi na kuacha sheria iwahukumu,” anaongeza Jumaa ambaye ni mwanafunzi wa sayansi ya siasa.

Mwalimu Mashaka wa Ubungo, Dar es Salaam, amepongeza Rais Samia angalau kuanza kuonyesha anavyochukia rushwa, ubadhirifu na wizi wa mali za umma.

Anasema sasa hatua inayofuata ni Rais Samia kuchukua hatua kwa kuwajibisha wote wanaotajwa kuhusika katika wizi wa mali za umma.

Halmashauri wizi mtupu

Sehemu nyingine ambayo imebainika kuwa na wizi mkubwa wa fedha za umma, - kama kawaida, ni halmashauri za wilaya, majiji na manisipaa, ambako Pambazuko linazo rekodi za ubadhirifu wa kutisha - kwa miaka nenda rudi.

Katika ripoti yake, CAG Kichere

amebainisha kuwepo kwa halmashauri 14 nchini ambazo zimepata hati chafu na zenye matatizo makubwa katika kutunza kumbukumbu za fedha.

Halmashari ya Ushetu, Mkoa wa Shinyanga kwa mwaka huu imekutwa na hati chafu. Hii maana yake ni kwamba kuna doa katika utendaji wake, hasa kwenye matumizi ya fedha.

Akitaja halmashauri zilizopata hati zenye mashaka ni Arusha DC, Babati DC, Bahi DC, Geuta DC, Geita DC, Geita TC, Kilindi DC, Mbinga TC, Musoma DC, Nkasi DC, Nyasa DC, Simanjiro DC, Songwe DC, Sumbawanga MC na Ushetu iliyoipata hati mbaya.

Vyama vya siasa

Mbali na maeneo mengi ya ofisi, taasisi na mashirika ya umma, pia kuna vyama vya siasa ambavyo hupokea fedha za umma, ambavyo vimepata hati zenye shaka kutokana na kuwa na ama matumizi mabaya ya fedha, kushindwa kutunza kumbukumbu ya fedha na mali.

Katika vyama vya siasa, Chama cha Sau kilipata hati chafu, Demokrasia Makini, UDP, Chama cha Wakulima vyote vilipata hati zisizoridhisha.

Mashirika ya umma

Katika mashirika ya umma ni Magazeti ya Serikali (TSN), Kampuni ya Mbolea, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega, Korogwe na Kyela-Kasumuru, Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Shirika la Masoko ya Kariakoo.

Tayari Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimeitaka serikali anayoongoza Rais Samia kuwachukulia hatua kali kwa waliohusika kwenye ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka katika taarifa ya CAG kwa mwaka 2021/22 na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Chama hicho tawala, kimesema kuwa na uhakika wa kuwepo kwa baadhi ya watumishi wa umma wasiokuwa waadilifu, hali inayosababisha serikali kushindwa kutoa huduma na kusukuma maendeleo ya wananchi.

Dhana Murua**Heshima ya mtu ni tabia njema**

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

HAKIKA ni kwamba watu wenye sifa hawapatikani kwa bahati, lazima upo mfumo wenye mwendelezo. Upo usemi kwamba mtu ni tabia. Kwa hiyo, watu hutengenezeka kwa kujengewa tabia.

Ina maana kwamba jamii inaweza kutengeneza watu wenye tabia njema au wenye tabia mbaya. Hivyo nirudie kusema tabia ni jumla ya ubora (qualities) na sifa za mtu zinazomtofautisha na watu wengine.

Mpango mzima wa malezi na makuzi yanalenga katika kutengeneza watu. Ni watu wa namna gani inategemea malengo na mpango mzima wa malezi.

Aristotle Nicomachus, mwanafalsafa wa Ugiriki, aliwahi kusema kwamba sifa za mtu hujengeka kwa yale anayojifunza na hujijengea tabia na mazoea kutoka kwa wazazi au walezi na jamii. Kwa hiyo, basi wazazi au walezi wazuri na jamii nzuri hutengeneza watu wazuri au vinginevyo kinyume chake.

Ni mfano wa jinsi mtoto anapoanza kufundishwa kupiga ngoma akifunzwa na mwalimu; na kwamba kadiri siku zinavyokwenda ndivyo maendeleo yake huonekana na vilevile huonekana tabia na uwezo wa mwalimu wake.

Mtu akifikia utu uzima, ana uhuru wa kuchagua kuwa na tabia njema au mbaya. Ikiwa wazazi au walezi na jamii hawana misingi na taratibu nzuri za malezi, basi itatengeneza watu wasiokuwa wazuri. Kwa hiyo, likifanyika kosa la malezi katika kizazi kimoja na kutengeneza watu wasio bora, hakika kizazi kinachofuata baada ya hicho nacho kitabomolewa.

Zaidi ya hayo, kizazi kibovu hakitengenezi kizazi kibovu tu, bali pia hakiwajengei kizazi kipya uwezo wa uchaguzi mzuri juu ya tabia zao. Inahitajika tabia nzuri kujenga tabia nzuri. Nini kifanyike ili kufanikisha mpango wa utengenezaji wa watu wenye



Tabia njema huansa kujengwa tangu utotoni (Picha ya Bezzia.com)

tabia nzuri?

Jamii isipokuwa na utaratibu mzuri wa malezi, basi kupata watu bora hubaki kuwa kwa kubahatisha. Eneo la malezi ni eneo ambalo linahitaji kufuatiliwa kwa karibu sana.

Ndipo hapo ambapo utafiti na tathmini za dhata juu ya maendeleo ya vizazi na jamii vinahitajika ili kupata taarifa sahihi za kuwezesha utengenezaji wa sheria, sera na mipango ya malezi bora.

Hii ina maana ufuatiliaji wa maisha na hali za familia, makuzi ya watoto na vijana; maendeleo katika mfumo mzima wa elimu na utaalamishaji; uwekaji wa vipimo na viwango vinavyokusudiwa kufikiwa na mipango yake; kupima na kuboresha uhusiano kati ya malezi ya familia na mifumo ya uelimishaji; na uhakiki wa tabia na uwezo wa wadau wote katika taasisi husika.

Mchakato huo ni muhimu kwani waundaji wa falsafa nzuri za siasa na uongozi bora hupatikana kutokana na kundi pana la watu.

Iwapo kundi hilo la watu halina ubora kutokana na maandalizi mavovu, itawezekanaje kujihakikishia kupata wasukaji wa mifumo safi na ya dhata ya siasa na uongozi? Tafakari!

Karibu Kamala Harris



Rais Samia akibadilishana mawazo na Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumsa na kiongozi wa Chama cha Chauma, Hashim Rungwe



Rais Samia akiwa na Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris wakati wa kuingia kwenye dhifa ya kitaifa aliyomwandalia mgeni wake. Harris alikuwa Tanzania kwa ziara rasmi

Tangazo

Pambazuko

**SASA
TUNAPOKEA
MATANGAZO**

**EWE
MFANYABIASHARA
NA MTOA HUDUMA,
ENDAPO UNAHITAJI
KUWAFIKIA WATEJA
WENGI ZAIDI BILA
KUJALI MIPAKA YA ENEO
ULILOPO, TANGAZA
NASI KWA**

Kuwasiliana kupitia: 0744 768 263
au Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Ustaarabu wa kimaadili historia ya Afrika

Na Digna DESIRATA

HISTORIA inayonyesha kuwa, upande lwa Kaskazini Mashariki mwa Misri, yaani katika Babeli ya kale, Kanuni ya Hammurabi (1750KK) ilikuwa kanuni ya maadili asilia, na inachukuliwa kuwa hati ya kwanza ya haki za raia.

Huko katikati ya Amerika Kusini, watu wa Inka nchini Peru wenyeji wanazyo seti ya sheria asilia ambazo ni za zamani sana, na zilitangulia mawasiliano yoyote yanayojulikana na Ulaya. Inajumuisha makatazo makuu matatu: “Sitaiba; “sitasema uongo”; na “sitakuwa mvivu.”

Hata miongoni mwa wawindaji na wakusanyaji wa matunda wa Afrika ya Kati, kulikuwa na sheria za kuongoza maisha ya pamoja.

Kwa ujumla, inaonekana kwamba kila jumuiya ingeachwa kwa hiari yao wenyewe ijiendeleze, ingetunga sheria fulani za kujiongoza, ili kuunda jamii iliyojulika.

Kwa kuzingatia mantiki hii, ni sawa pia kusema kwamba, Waafrika pia walikuwa na kanuni zao asilia kwa ajili ya kuongoza maisha ya pamoja. Sheria hizo zilizafanuliwa vema katika dola ya kale ya Misri iliyojulikana kama “Kemeti,” kule alikokulia Nabii Musa.

Kwa mujibu wa wanahistoria, sheria hizo za Kifrika ndio asili ya Amri Kumi za Wakristo ambazo Musa anatajwa “kupokea kutoka kwa Mungu” akiwa Mlima Sinai, ulioko nchini Misri. Ufafanuzi unafuata.

Musa alikuwa Mwafrika Historia inaonyesha kwamba Musa alikuwa mtu Mweusi wa Afrika aliyezaliwa katika dola ya Kemet ya kale (Misri) wakati wa utawala wa Pharoah Harimbab (1340-1320 B.K.).

Musa alitumia muda mwingi wa maisha yake huko Misri na kumwoa mwanamke Mwithiopia aitwaye Zipora. Walikuwa na wana wawili Gershoni na Eliyeri.

Kulingana na ushahidi wa kimaandishi, Musa ambaye alizaliwa kutoka kabila la Lawi, alikolewa kimiujiza na dada yake



Ramani ya Afrika

Miriam alipokuwa akielea kwenye Mto Naili katika kikapu cha mitende.

Alifichwa Kusini mwa Mto Naili na mama yake kwa sababu Farao wa Misri Ramses I alikuwa akiwaua wanaume wote wa Kiebrania waliozaliwa katika ufalme wote.

Ukweli ni kwamba akiwa Kuhani Mkuu wakati wa utawala wa Farao Akhneton (Nasaba ya XXV, 1370-1352 B.K.), Musa aliibuka na kuwa mtu mwenye ujuzi “Maungamo 42 ya Maadili ya Wamisri” pamoja na “Aina 10 za dhambi” zilizokuwa zinakatazwa katika dola ya Kemet ya kale (Misri).

Pia alikuwa mfuasi wa Imani ya Mungu Mmoja ambayo Farao Akhneton alikuwa ameianzisha kwa watu watu.

Hivyo ndivyo Biblia Takatifu, katika kitabu cha Matendo 7:22, inavyosema, yaani: “Musa alifundishwa katika hekima yote ya Wamisri na alikuwa hodari katika maneno na matendo.”

Kimsingi basi, hadi anafika Mashariki mwa Misri kwenye Mlima Sinai, Musa alikuwa anamwabudu Amun-Ra, Mungu wa Jua wa Misri ya Kale.

Kuzaliwa kwa Amri Kumi

Hatimaye, ilikuwa rahisi sana kwa Musa kuanzisha dini mpya kwa ajili ya

Uchambuzi

Ustaarabu wa kimaadili historia ya Afrika

Inatoka Uk. 15

watu wake kama matokeo ya elimu yake ya kiroho na mafunzo huko kwenye dola ya Kemet Magharibi (Misri).

Kwa ajili hii, Musa alichuja “Matamko 42 ya Maadili ya Wamisri,” akaunda “Amri Kumi” na akaendelea kukumbatia dhana ya Imani ya Mungu Mmoja.

Musa alitumia dhana ya moto kupokea “Amri Kumi” kwa sababu katika Kemet ya kale (Misri) nguvu ya kiroho ya Mungu iliwakilishwa na moto.

Kwa maneno mengine, dini ya wafuasi wa Musa siku hizi ina asili ya Kiafrika, ukiwemo Ukristo uliolirithi Agano la Kale.

Musa akimbia hasira ya Farao

Ushahidi kwenye rekodi za kimaandishi unaonyesha kwamba, Musa alilazimika kukimbia hasira ya Farao Ramses II kwa sababu alikuwa amemua askari wa Ramses.

Kwa hiyo, Musa akapanga “kuwaondoa” Wamisri wenzake wenye asili ya Kiebrania kutoka Magharibi ya Misri hadi Misri ya Mashariki, yaani, kutoka mwisho wa Delta ya Aswan ya Mto Naili hadi Mlima Sinai.

Ni sahihi kufikiri kwamba, mfalme Ramses II alimkimbiza Musa katika jangwani lote la Misri ili kulipiza kisasi kwa sababu ya askari wake ambaye Musa alimua.

Yaani, Musa alikuwa anashitakiwa kwa mauaji. Hivyo, Musa alikuwa akikimbia kutoka eneo la uhalifu wake huko katika dola ya Kemet (Misri).

Kwa maneno mengine, Musa alikuwa akijaribu kuwakomboa watu wake kutokana na adhabu ambayo uhalifu wake ungesababisha.

Katika Misri ya kale kwa wakati huo, Wayahudi, ambao hapo awali waliitwa Waebrania, walikuwa wamehama kutoka Asia wakikimbia janga la njaa.

Hakuna ushahidi kwamba Wayahudi hawa wa Kiasia walikuwa na elimu rasmi ya kiwango kwa njia yoyote inayolinganishwa na ile ambayo Waafrika wa kiasili wa Misri walikuwa wamekuza.

Wala hakuna ushahidi wowote kwamba walikuwa na kanuni za maadili



Afrika

na maadili ambazo zilikuwa kinyume, au kuunga mkono, za wale waliokutana nao katika nchi ya Kemeti, yaani Misri ya Kale. Wayahudi hawa walikuwa wachungaji tu walipoingia Misri.

Wayahudi waliingia nchini Misri karibu mwaka 1632 KK na kukaa humo mpaka walipoanza kuondoka mwaka 1232 BK, wakati wa utawala wa mfalme Ramses II, aliyetawala 1279KK hadi mwaka 1212 KK

Wamisri hawakukubali tu kaka na dada zao wa Kiasia, Waebrania, kama watu sawa lakini pia waliwajumuisha katika kila nyanja ya jamii ya Wamisri.

Kabla ya muungano huo uliokubalika, Wayahudi hao hawakuwa wameanzisha serikali popote, isipokuwa vikundi vya makabila.

Katika kipindi hicho, tayari piramidi kuu zilikuwa tayari zimejengwa na Farao Khufu, Khafra na Menkara kwenye uwanda wa Giza, kipindi ambacho kilipanuka tangu 2680KK hadi 2258 KK.

Matamko 42 ya Maadili ya Wamisri

Ni kati kati ya ustaarabu huu, kulizaliwa “Matamko 42 ya Maadili ya Wamisri” yanayopatikana katika maandiko matakatifu ya kiroho yaliyoandikwa kwenye kuta za Hekalu la Unas katika Misri ya kale.

Matamko hayo 42 ndizo kanuni za maadili asili za kiroho za Waafrika wa

Endelea Uk. 17

Uchambuzi

Ustaarabu wa kimaadili historia ya Afrika

Inatoka Uk. 16

Misri. Matamko hayo ni kama ifuatavyo:

(1) Sikufanya dhambi; (2) Sijafanya ujambazi; (3) Sijaiba; (4) Sikuuu, sikufanya ubaya; (5) Sikudhulumu sadaka; (6) Sijatelekeza majukumu; (7) Sikumteka nyara mwindaji; (8) Sikusema uongo; (9) Sikunyang'anya chakula; na (10) sikusababisha mateso;

Matamko mengine ni, (11) sikufanya uasherati; (12) Sikumtoa mtu machozi; (13) Sikufanya hila; (14) Sijakiuka haki ya mtu; (15) Sikufanya hila; (16) Sikuharibu shamba la mtu; (17) Sikuwa msikilizaji wa siri za watu; (18) Sikufanya umbea; (19) Sikukasirika na kughadhibika ila kwa haki. (20) Sikuzini;

Pia, matamko mengine ni, (21) Sikumnajisi mke wa mtu; (22) Sikujitia unajisi; (23) Sikusababisha hofu; (24) Sikukosa uadilifu; (25) Sikuwaka hasira; (26) Sikuziba masikio yangu juu ya maneno ya haki. (27) Sikusababisha huzuni; (28) Sikufanya jeuri; (29) Sikuchochea ugomvi; (30) Sikuhukumu kwa haraka;

Kadhalika matamko mengine ni, (31) msikilizaji wa majungu; (32) Sikufanya uchochezi; (33) Sikufanya ubaya; (34) Sikumlaani Mfalme; (35) Sikuchafua maji; (36) Sikusema kwa dharau; (37) Sikumlaani mfungaji; (38) Sijaiba; (39) Sikuzidhulumu sadaka za mfumaji; (40) Sikuteka nyara sadaka za wafu waliobarikiwa.

Na matamko mengine ni haya, (41) Sikukinajisi chakula cha mtoto mchanga, wala sijamtenda dhambi mvuvi wa mji wangu wa asili; na (42) Sikuwachinja wanyama wa nyandari kwa nia mbaya.

“Matamko 42 ya Maadili ya Wamisri”

yanawakilisha kanuni za kwanza za maadili zilizobuniwa na Waafrika wa Misri. Waafrika walibuni kanuni hizi za maadili katika zama za kabla ya Kristo. Matamko haya yalitengenezwa kabla ya kuwa na Biblia Takatifu ya Kikristo na kabla ya kuwepo kwa Kurani ya Kiislamu.

Kwa ufupi, iliwachukua Waafrika wa kale vizazi hamsini (50) au miaka 1,200 kuendeleza kanuni hizi za maadili na kiroho.

Sababu kwa nini kulikuwa na “Matangazo 42 ya kutokuwa na hatia” ni kwa sababu kulikuwa na Wilaya 42 katika Kemet ya kale wakati huo.


Ukarabati wa Matamko 42

Musa wa Misri alipeleka “Matamko 42 ya Maadili ya Wamisri” kwa watu wake. Lakini, ilimbidi azibadilishe kwa sababu alikuwa akizungumza na watu waliokuwa wakiishi katika mapango na vilima vya Ulaya na ambao hawakuwa wameishi maisha ya kiroho.

Kwa hivyo, Musa ilimbidi kubadilisha matamko ya Kimisri yaliyianza kwa maneno “Sikufanya moja, mbili, tatu” hadi kuwa amri zinazoanza kwa neno “Usifanye moja, mbili, tatu.”

Wakati huo wa Musa, kulikuwa na aina kumi (10) za dhambi katika Misri. Hivyo, hizi zikawa kategoria za dhambi ambazo

Endelea Uk. 18



Afrika ilikuwa na utaalamu wake mkubwa kama mapiramidi haya ya Misri yanavyoonekana kujengwa bila wasungu

Uchambuzi**Ustaarabu wa kimaadili historia ya Afrika****Inatoka Uk. 17**

Musa, Mwaafrika, alitumia kama msingi wa kutunga zile “Amri Kumi.”

Makundi kumi ya dhambi katika Misri ya kale ni kama ifuatavyo: (1) Dhambi za jumla dhidi ya watu, (2) Uhalifu dhidi ya mtu, (3) Uhalifu dhidi ya Miungu, (4) Uhalifu dhidi ya Mfalme, (5) Uhalifu dhidi ya Waliokufa, (6) Uhalifu dhidi ya wanyama, (7) Uhalifu dhidi ya Mali, (8) Ulaghai, (9) Makosa ya maadili na tabia kundi la kwanza; na (10) Makosa ya maadili na tabia kundi la pili.

Ulinganisho wa matamko 42 na amri 10

Kwa hivyo, mazingira haya yakamshawishi Musa kuchuja na kufupisha matamko 42 hadi amri 10. Hivi ndivyo “Amri Kumi” za kidini za Ukristo zilivyozalwa katika Afrika, na ulinganisho wake ni kama ifyatavyo:

Kuna (1) Mimi ndimi Bwana, Mungu wako, Usiwe na miungu mingine ila mimi (inatokana na tamko 41); (2) Usijifanyie sanamu ya kuchonga (inatokana na tamko 7, 37, 41); (3) Usilitaje bure jina la Bwana wao Mungu (inatokana na tamko 7, 37, 41); (4) Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase (inatokana na tamko 1, 12, 28);

Kuna (5) Waheshimu baba yako na mama yako (inatokana na tamko 1, 12, 28); (6) Usiue (inatokana na tamko 4); (7) Usizini (inatokana na tamko 11, 20, 21); (8) Usiibe (inatokana na tamko 2, 3, 5, 6, 7, 9, 39, 40);

Pia kuna, (9) Usitoe ushahidi wa

uwongo dhidi ya jirani yako (inatokana na tamko 8, 13, 18, 29); na (10) Usitamani nyumba au mke wa jirani yako (inatokana na tamko 13, 20, 21, 29, 33).

Kwa maneno mengine, Amri Kumi za siku hizi za Wakristo hazikuletwa Afrika na Wamisinari, bali zilianzia Afrika zikaenda huko Ulaya, na kasha kurudi kwake Afrika.

Kama ambavyo Ugriki ya Kale ni kitovu cha ustaarabu wa Ulaya, au kama ambavyo Roma ni kitovu cha Ukristo wa Ulaya, vivyo hivyo, Misri ya Kale ni kitovu cha ustaarabu wa Afrika.

Kwa kuhitimisha basi, tunaweza kusema kuwa, katika zama za kabla ya Kristo, Afrika ilijulikana kama “Nchi ya watu wa kiroho.” Lakini, kwa sababu za kihistoria, Waafrika wamepoteza hali yao ya kiroho ya asili.

Kwa hivyo, katika milenia hii mpya ya karne ya 21, Waafrika katika Bara la Afrika na Wanadayaspora wanapaswa kurejesha, kukamata upya, kuunganisha upya, kupanga upya na kuigiza upya hali yao ya kiroho kama silaha yenye nguvu zaidi katika ghala lao la silaha ili kuendelea kuishi na kujiwezesha wenyewe.

Yaani, Waafrika tunajitosheleza kimaadili, kiasi kwamba, hawahitaji “kutakatifuzwa” wala “kustaarabishwa” na Wazungu, Wamarekani wala Waarabu.

Kwa kuzingatia historia hii, makala yajayo yatajadili kwa ukamilifu mtazamo wa Waafrika kuhusu maadili asilia.





Na Mwandishi WETU

MIONGO kadhaa iliyopita, ilikuwa kama mwiko kwa timu za Tanzania kusonga mbele kwenye michuano mikubwa ya kimataifa.

Mara nyingi, timu za Tanzania, hasa Simba na Yanga ambazo zimeweka historia ya kuwa vinara wa ligi za soka, zimekuwa zikikwama kusonga zaidi kwenye michuano ya Afrika, mabara na hata dunia. Mara nyingi zimekuwa zikitolewa hatua za awali.

Hata hivyo, kwa mwaka huu, timu kubwa za Simba na Yanga zinaelekea kuvunja mwiko huo kwa kuonyesha dalili za kusonga kwenye hatua za juu za michuano ya soka Afrika.

Katika kudhihirisha hilo, jana, Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya TP Mazembe wakiwa nchini mwao Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Mchezo wa kwanza kwa timu hizo ulichezwa Dar es Salaam, Tanzania na Yanga kuibuka washindi kwa mabao 3-1.

Ushindi huo sasa unaiweka timu hiyo ya Tanzania katika nafasi nzuri ya kuendelea na michuano hiyo ya Afrika ambayo inatambuliwa na Shirikisho la

Soka Duniani (FIFA).

Mchezo wa jana ulikuwa wa kufunga dimba kwa kundi D na kwamba bao la Yanga lilifungwa na Farid Mussa Malik katika dakika ya 63.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kufikisha pointi 13, huku ikiwa ianongoza kundi hilo hadi tunapoenda mitamboni. Timu nyingine inayoweza kuiondoa Yanga kileleni ni US Monastir ambayo ilitakiwa kupata ushindi wa kuanzia mabao matatu katika mchezo wake dhidi ya Real Bamako ya Mali.

Mchezo huo ulitarajiwa kuanza saa 5:00 usiku wa jana wakati Pambazuko likiwa mitamboni. Mechi hiyo ilipangwa kufanyika katika Jiji la Tunis, Tunisia katika dimba la Hammadi Agrebi.

Kitendo cha kumaliza kundi ikiwa nafasi ya kwanza itaipa faida ya kukutana na timu zilizoshika nafasi ya pili, pia itaanzia ugenini na kumalizia nyumbani.

Hatua ya robo fainali ya michuano hii, ambayo Yanga imejihakikishia nafasi, inatarajiwa kufanyika Aprili 05, katika Jiji la Cairo, Misri. Inatarajiwa kuwa mechi za raundi ya kwanza zitaanza Aprili 23, 2023 na marudiano yatakuwa Aprili 30.

MAMA AGEUZWA CHAKULA...



Mwana wa nyani hana habari kwamba mama yake tayari amekufa na ndiyo chakula cha chui muda mfupi ujao. Inasikitisha, lakini ndiyo ikolojia. Picha hii imechotwa kutoka mtandao wa intaneti na mpigapigapicha hakutambulika wala sehemu ilipochukuliwa.

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 0000448.

